NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Riḍván 2020

Kwa Wabahá’í wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Uhalisia wa aina mbili unaojitokeza umetuchochea tuwaandikie maneno haya. Uhalisia wa kwanza ni utambuzi unaoongezeka kote ulimwenguni wa hatari zinazoonekana kubwa na za kutisha ziletwazo na gonjwa hatari la homa ya mapafu linalosababishwa na virusi vya corona. Katika nchi nyingi, licha ya jitihada kubwa na za makusudi za pamoja za kuzuia janga hili, hali tayari ni tete, ikileta maafa kwa familia na watu binafsi na kuitumbukiza jamii nzima katika mfadhaiko. Mawimbi ya mateso na huzuni yanakunjuka eneo moja baada ya lingine, na yatayadhoofisha mataifa mbalimbali, kwa nyakati mbalimbali, kwa njia mbalimbali.

Uhalisia wa pili, ule ambao huonekana dhahiri zaidi kila siku, ni nguvu thabiti na isiyopunguka ya ulimwengu wa Kibahá’í mbele ya changamoto ambayo haina mfano wake katika kumbukumbu zilizopo. Muitikio wenu umekuwa wa kipekee. Tulipowaandikia wakati wa Naw-Rúz mwezi mmoja uliopita, tulikuwa na shauku ya kusisitizia sifa za kuvutia zinazooneshwa na jumuiya ambazo mtindo wake wa kawaida wa shughuli umevurugwa. Yale yote yaliyotukia katika majuma ya kati, wakati ambapo marafiki wengi hawakuwa na budi kukubaliana na vizuizi vilivyoongezeka kiukali, yameongeza tu hisia zetu za uvutiwaji. Zikijifunza kutokana na tajiriba iliyopatikana katika sehemu zingine za ulimwengu, baadhi ya jumuiya zimepata njia salama na za kiubunifu za kuinua ufahamu wa mahitaji ya afya ya umma ndani ya jamii. Uangalifu maalum unawekwa kwa wale ambao wapo katika hatari zaidi kupata virusi na dhiki za kiuchumi zitokanazo na ueneaji wake; ari zilizoandikwa katika Huduma ya Habari ya Ulimwengu wa Kibahá’í (Bahá’í World News Service) kuhusiana na hili ni konzi tu ya idadi isiyohesabika inayoendelea. Hizi hushamirishwa na jitihada za kuchunguza, kuendeleza na kukuza zile sifa za kiroho ambazo huhitajika zaidi katika wakati huu. Nyingi ya jitihada hizo kiulazima zinatokea katika ngazi za familia au katika upekee, lakini pale ambapo hali huruhusu au vyombo vya mawasiliano hufanya iwezekane, hali ya mshikamano usio wa kawaida unalelewa kwa bidii miongoni mwa roho zinazoshirikiana hali zifananazo. Nguvu ya maisha ya kijumuiya, muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya wote, haitadhibitiwa.

Mioyo yetu imeinuliwa kwa kuona jinsi Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa kwa uwezo, majemadari wasiochoka wa Jeshi la Mwanga, yalivyoziongoza jumuiya zao na kubumba muitikio wao kwa janga hili. Yamekuwa yakisaidiwa vyema na Washauri na wasaidizi wao ambao, kama kawaida, kishujaa wameinua juu kiwango cha huduma yenye upendo. Wakati wakibakia waliofahamishwa vyema kuhusiana na hali zibadilikazo kwa haraka mara kwa mara katika nchi zao, Mabaraza yamefanya yale maandalizi ya lazima kwa ajili ya kusimamia shughuli za Hoja na hususan kwa ajili ya kuendesha chaguzi, pale ambapo haya huwezekana. Kupitia mawasiliano ya mara kwa

mara, asasi na mawakala zimetoa ushauri wa busara, zikiwaondoa shaka, na kuwatia moyo bila kukoma. Katika mazingira mengi, wameanza pia kubaini mada zenye kujenga ambazo zinaibuka kutoka katika mijadala inayofunguliwa katika jamii zao. Matarajio tuliyoyaeleza katika ujumbe wetu wa Naw-Rúz, kwamba jaribu hili la ustahimilifu wa jamii ya binadamu lingeipa umaizi mkubwa zaidi tayari linatambuliwa. Viongozi, watu mashuhuri wenye fikra, na watoa maoni wameanza kuchunguza dhana za kimsingi na matamanio ya kiujasiri ambayo, kwa nyakati za hivi karibuni, kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakikosekana katika mijadala ya kijamii. Kwa wakati huu hizi ni dalili za awali tu, lakini huonesha uwezekano kwamba wakati wa utambuzi wa pamoja unaweza kuwa katika upeo wetu.

Faraja tunayoipata tuonapo uthabiti wa ulimwengu wa Kibahá'í ukijidhihirisha wenyewe kivitendo inapunguzwa na huzuni yetu kwa madhara ya gonjwa hili hatari lililoenea pote kwa jamii ya binadamu. Ole, tunatambua kwamba waumini na washirika wao pia hushiriki mateso haya. Umbali kutoka kwa marafiki na ndugu ambao, kufuatia mahitaji ya usalama wa umma, watu wengi sana ulimwenguni sasa wanauendeleza, kwa baadhi, utatoa njia kwa mtengano wa kudumu. Kila mapambazuko inaonekana yakini kwamba maumivu makali yatastahimiliwa zaidi kabla machweo ya jua. Hebu ahadi ya muungano tena katika falme za milele itoe kitulizo kwa wale ambao hupoteza wapendwa wao. Tunasali kwa ajili ya ahueni ya mioyo yao, na ili rehema na neema za Mungu ziwazunguke wale ambao elimu yao, maisha yao, nyumba zao au hata njia zao zenyewe za kujipatia riziki zinawekwa hatarini. Kwenu nyinyi, na kwa wale mnaowapenda sana, na kwa washirika wenu wote, tunamuomba Bahá'u'lláh na kusihi baraka Zake na fadhili.

Japokuwa njia ambayo lazima isafiriwe ni ndefu na yenye sulubu ihitajiyo nguvu, tuna imani kubwa mno katika ushupavu wenu na dhamiri yenu kuona mwisho wa safari. Mnachota kutoka katika ghala ya matumaini, imani, na ukarimu, mkitanguliza mahitaji ya wengine kabla ya yenu wenyewe, mkiwawezesha wale ambao wamenyimwa waweze kusitawishwa kiroho, wale ambao wana kiu iongezekayo kwa ajili ya majibu kutoshelezwa, na wale ambao hutamani kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu waweze kupewa zana. Kutoka kwa wafuasi waliojifunga kibwebwe wa Uzuri Mkamilifu, ni vipi tungetegemea pungufu ya haya?

Umesainiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu